

### ❖ Ziwe na ukubwa wa wastani

Mbegu bora zinatakiwa ziwe na ukubwa wa wastani, zisiwe ndogo au kubwa sana bali ukubwa wake uwe unaolingana na ukubwa wa yai. Mbegu ikiwa ya maumbo makubwa sana itaongeza gharama za uzarishaji, maana mahitaji ya mbegu kwa eneo husika yatakuwa kuliko kiwango kinachoshauriwa ukitumia kitaalam. Vile vile mbegu ndogo ndogo sana uotaji wake huwa sio mzuri kwani zinakuwa hazina umbo zuri la kuweza kuhifadhi chakula chake kitakachosaidia kuleta nguvu ya uotaji. Pia mbegu zitatumika chache sana kuliko kiasi kinachoshauriwa na wataalam.

### ❖ Ziwe na ukinzani na magonjwa na wadudu.

Mbegu bora zinatakiwa ziwe na ukinzani na magonjwa kama vile ukungu na bakteria mnyauko. Shamba lenye wadudu na magonjwa hupelekea kupungua kwa mavuno mpaka kiwango cha asilimia mia moja. Hivo mkulima tumia mbegu bora yenye ukinzani huo.

## SEHEMU SAHIHI ZA KUPATA MBEGU BORA ZA VIAZI MVIRINGO

- i. Vituo vyote vya taasisi ya utafiti kilimo Tanzania (TARI-Uyole, TARI-Kifyulilo na TARI-Tengeru)
- ii. Vikundi vya wakulima wa mbegu chini ya uangalizi wa watafiti na wathibiti wa mbegu (TOSCI)
- iii. Wakulima binafsi waliochaguliwa kuzalisha mbegu zilizoazimiwa ubora yaani QDS chini ya uangalizi wa vituo vya utafiti (TARI) na TOSCI.
- iv. Makampuni ya mbegu chini ya masharti na uangalizi wa vituo vya utafiti (TARI) na TOSCI.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

### **MENEJA**

**TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO**

**TARI - KIFYULILO**

**S.L.P 93 MUFINDI**

**IRINGA**

**SIMU: 0765176040/0769492549**

**Baruapepe: [cmkifyulilo@tari.go.tz](mailto:cmkifyulilo@tari.go.tz)**

**Tovuti: [www.tari.go.tz](http://www.tari.go.tz)**

## TAASISI YA UTAFITI WA

## KILIMO TANZANIA

(TARI)



## TAMBUA SIFA ZA MBEGU

## BORA ZA VIAZI

## MVIRINGO



## UTANGULIZI

Viazi mviringo ni zao muhimu la chakula na biashara ambalo idadi ya wahitaji inaongezeka kila siku nchini Tanzania. Hapa nchini viazi hustawi vizuri zaidi sehemu za miinuko zenye mvua nyingi na baridi kali.

## MAENEO AMBAYO VIAZI MVIRINGO HUSTAWI

Hapa nchini maeneo ambayo zao la viazi mviringo hufanya vizuri kutokana na mvua nyingi na baridi kali ni kama wilaya za Rungwe, Mbeya vijijini, Ileje, Makete, Njombe, Mufindi, Mbinga, Sumbawanga na maeneo ya milima ya Uluguru, milima ya Usambara, West Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Mara.

## UMUHIMU WA MBEGU BORA

Ili kukuza pato la mkulima ni lazima kuzungumzia mavuno yenye tija ambayo hutokana na matumizi ya mbinu sahihi za kilimo. Moja yambinu sahihi za kilimo ni matumizi ya mbegu bora hivyo mbegu bora husaidia kuongeza mavuno yenye tija kwa mkulima kutokana na sifa mbalimbali ambazo zinakuwa zimeboreshwa na kugunduliwa na watafiti na waganduzi waliobobea katika masuala ya kilimo.

## SIFA ZA MBEGU BORA ZA VIAZI MVIRINGO

Sifa za mbegu bora za viazi mviringo, ni zile zenye kukidhi vigezo vifuatavyo:

### ❖ **Zenye kutoa mazao mengi zaidi kutoka kwenye shina moja**

Mbegu bora zinakuwa na idadi kubwa ya mazao katika shina moja nah ii ni kiashiria cha kuonesha wingi au uchache wa mavuno shambani.

### ❖ **Zisiwe na magonjwa wala wadudu**

Ni muhimu mbegu zisiwe na magonjwa wala wadudu ili kuepuka magonjwa na wadudu kuonekana kwenye mazao yako maana uwepo wa magonjwa na wadudu hupunguza mavuno mpaka kiwango cha asilimia mia moja.

### ❖ **Mbegu ziwe za aina moja**

Ni vizuri mbegu hizo zote ziwe za aina moja kwakuwa kila mbegu ina sifa za upekee kulingana na matakwa ya mtafiti au mgunduzi husika kulingana na mahitaji ya walengwa wa mbegu hiyo.

Hivyo mkulima anapopanda mbegu za aina mbalimbali humuongezea gharama za uzalishaji kwa kupambana na magonjwa na wadudu maana kila mbegu ina ukinzani wa kipekee kwa magonjwa na wadudu hivyo, matumizi yz aina moja ya mbegu hurahisisha kujua mbegu hiyo inatoa mavuno kiasi gani na ni kwa kiasi gani ina ukinzani kwenye magonjwa na wadudu.

### ❖ **Ziwe zimechipua vizuri.**

Mbegu bora zinatakiwa ziwe zimechipua vizuri ili kuendana na muda sahihi wa kuota baada ya kupandwa shambani kwa kina cha sentimeta 15 pia machipukizi yaliyo chipua vizuri huashiria mavuno mengi kwani idadi na afya ya miche hutegemea zaidi hali ya machipukizi hayo.

### ❖ **Ziwe na machipukizi mengi.**

Mbegu bora ni ile yenye machipukizi mengi ya kutosha kuanzia 4 mpaka 7, hii ina maanisha kwamba karibu kila jicho kwenye kiazzi liwe na chipukizi. Idadi kubwa ya machipukizi ni kiashirio kizuri kuwa uotaji wa mbegu shambani utakuwa kwa kiwango kikubwa na kupelekea mavuno kuwa mengi na yenye tija.